**MUNGU ANA MPANGO**

(Sehemu ya Tatu ya Mfululizo huu)

Na Jacquelyn Fedor

Ilitafsiriwa Na David Odhiambo

Tofauti na dini na makundi mengi tunayopata ulimwenguni leo, kutakuwa na kanisa moja tu katika Ufalme wa Mungu. Anamwona kama Bibi-arusi Wake asiye na dosari, mke mwaminifu.

**Ufunuo 21:9-11**

9 Kisha mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba
vilivyojaa mapigo saba ya mwisho akaja kwangu, akazungumza nami,
akisema, "Njoo, nitakuonyesha bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo".
10 Naye akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu,
akanionyesha ule mji mkuu, Yerusalemu takatifu, ukishuka kutoka mbinguni
kwa Mungu,
11 wenye utukufu wa Mungu. Nuru yake ilikuwa kama jiwe la thamani sana,
kama jiwe la yaspi, angavu kama bilauri.

Aliachiliwa aje msalabani, au niseme, Alimruhusu adui kupitia mwanadamu wa kimwili kumweka huru! Hawa alipochukuliwa kutoka upande wa Adamu, kanisa lilizaliwa wakati upanga wa adui ulipopenya ubavu wa Bwana, ukimuweka huru kama maji na damu yalivyotoka. Mpango wa Mungu kwa

ajili yake ni upi?

Hebu tuangalie ukweli. Akiwa amezaliwa kwa damu ya Adamu, Roho Mtakatifu humvuta na kumtambulisha kwa Yesu, Mti wa Uzima. Anajua wengi watamchagua kuwa Bwana wao. Hawatataka kubaki katika hali ya kushindwa waliyo kuwa wazao wa Adamu na kuishi maisha yao kama waliolaaniwa. Wakitamani kuanza maisha upya, wakati huu pamoja Naye, wanachagua kuzaliwa tena. Baada ya kufafanuliwa kwao kwamba utu wao wa kimwili unaweza kufa katika kifo chake katika ubatizo, na utu mpya wa kiroho kufufuliwa kupitia ufufuo wake ambao unaweza kuuona Ufalme, wanatumaini watachagua maisha mapya. Hiyo ndiyo maji yanafananisha.

**Warumi 6:4-6**

4 Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi
kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo na
sisi tuenende katika upya wa uzima.
5 Kwa maana ikiwa tumeunga pamoja katika mfano wa mauti yake, bila
shaka sisi nasi tutaunganishwa katika mfano wa kufufuka kwake;
6 tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili
mwili wa dhambi uharibike, ili tusiwe tena watumwa wa dhambi.

Tulipojifunza katika sehemu moja ya mfululizo huu, kwa njia ya dhabihu ya damu yake pamoja na uhai wake ndani yake, wangesamehewa dhambi zote,

na kupitia ushirika waingie agano Lake kama warithi wa wote alionao kama Bibi-arusi Wake, jamaa zake. Wao pia wangekuwa wa milele kama vile Yeye ni wa milele, na kustahiki kurudi kwa Kristo bustani. Pia, kupitia damu yake na zawadi ya toba, Bibi-arusi angeweza kuwekwa mtakatifu milele, tofauti na Hawa ambaye alikuwa na kifuniko cha Adamu tu.

**Waefeso 5:26-27** inaeleza:

26 ili yeye (Yesu) alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno,

27 apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; awe mtakatifu na asiye na dosari.

Hivi ndivyo damu ilivyoashiri.

Jambo lingine lilitokea vilevile Neno, upanga wa Kweli, au Kristo Mwenyewe, alichomwa na upanga wa adui. Ukuu, haki ya Ubwana lilikuwa suala la kupingwa, lakini pia, ushindi wa Kristo dhidi ya Shetani ulikuwa wa lazima kwa wanadamu kuruhusiwa kuingia kwenye bustani kwa mara nyingine tena! Kumbuka, upanga ulikuwa umewekwa kati ya mwanadamu na Mti wa Uzima.

**Mwanzo 3:24**

24 Akamfukuza huyo mtu; akaweka makerubi upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia

ya mti wa uzima.

Kwa sababu ya pigo hili la mwisho msalabani, upanga uliozuia njia ya kwenda Paradiso uliacha ulinzi wake wakati wa kufutwa kwa dhambi ya Adamu. Haki ya kurudisha mzunguko kamili kwenye bustani ya asili sasa ilitolewa kwa wale wote ambao wangeingia katika agano lake la damu.

Yote yalikuwa ni sehemu ya mpango wa asili wa Mungu. Yesu alipotolewa dhabihu, Neno la Mungu, Upanga Wake ulishinda maarifa ambayo Hawa alichagua, na akainuka kwa ushindi juu ya Mti wa Mema na Ubaya.

**Waebrania 4:12**

12 Kwa maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga wenye makali kuwili (wa adui), tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; mawazo na makusudio ya moyo.

Maarifa ya Mungu yalishinda maarifa ya kiakili, maarifa yaliyotokana na uzoefu au mawazo ya kiumbe mwingine. Alitengeneza njia kwa Bibi-arusi kuchagua Hekima kutoka kwa Mti wa Uzima wakati huu, kuwa Kanisa jipya tukufu, Hawa wa mwisho.

Sasa Mungu aliweza kufungua ujumbe kwa kanisa ambalo Danieli aliambiwa

afunge mpaka mwisho. Mkewe angeweza kulielewa kabisa, angefikiri mawazo Yake, kufanya mambo kulingana na mipango Yake, njia Yake.

**Danieli 12:9-10**

9 Naye akasema, “Nenda zako, Danieli, kwa maana maneno haya
yamefungwa na kutiwa muhuri mpaka wakati wa mwisho.
10 Wengi watatakaswa, na kufanywa weupe, na kusafishwa, lakini waovu
watafanya hivyo kwa uovu, na hakuna hata mmoja wa waovu atakayo elewa,
bali wenye hekima wataelewa.

Habari inatolewa kutoka katika gombo lililotiwa muhuri na Bwana kupitia wafunuaji Wake, kwa serikali Yake. Wao nao humlisha Bibi-arusi ujuzi huu ili aweze kufahamu ahadi katika maagano na kutoa mwelekeo wa ulinzi wake katika wakati huu wa mwisho.

**Ufunuo 5:1-5**

1 Kisha nikaona katika mkono wa kulia wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti
cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa muhuri saba.
2 Kisha nikaona malaika mwenye nguvu akitangaza kwa sauti kuu, “Ni nani
anayestahili kukifungua hicho kitabu na kuzivunja muhuri zake?”
3 Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala duniani, wala chini ya nchi,
aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama.
4 Kwa hiyo nikalia sana, kwa sababu hakuna yeyote aliyepatikana

anayestahili kukifungua kitabu hicho cha kukunjwa, au kukitazama.
5 Lakini mmoja wa wale wazee akaniambia, “Usilie. Tazama, Simba wa kabila ya Yuda, Shina la Daudi, ameshinda kukifungua hicho kitabu na kuzivunja lakiri zake saba.” (Yeye, Yesu, alikuwa ameshinda heshima hii pale msalabani.)

Bibi-arusi analindwa dhidi ya adui wakati yaliyomo ndani ya mihuri yanapofunguliwa duniani. Shetani hataruhusiwa kulipiza kisasi dhidi yake na ghadhabu ya Mungu itazuiliwa kutoka kwake. Yesu ni shujaa wake, Mkuu wake, bingwa wake juu ya farasi mweupe.

**Ufunuo 19:13-16** pia inatuambia,
13 Alikuwa amevishwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake anaitwa Neno la Mungu.
14 Na majeshi ya mbinguni, waliovaa kitani nzuri, nyeupe, safi, wakamfuata, wamepanda farasi weupe.
15 Sasa upanga mkali hutoka kinywani mwake, ili awapige mataifa kwa huo. Naye mwenyewe atawachunga kwa fimbo ya chuma. Yeye mwenyewe anakanyaga shinikizo la divai ya ukali na ghadhabu ya Mungu Mwenyezi.
16 Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake: MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA.

Vazi hilo lililotiwa madoa ya damu limefunikwa kwa ubinadamu leo,

likitulinda, linafunika dhambi zetu, lakini pia linatufanya kuwa wenye haki ili Shetani hana haki kwetu. Mfalme anatukabidhi fimbo ya haki, ikituruhusu kurejeshwa, kufanywa upya, kukubaliwa kama Bibi-arusi wake. Yote ilikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu.

**Waebrania 1:8**

8 Lakini kwa Mwana asema: “Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, ni cha milele na milele; fimbo ya haki ni fimbo ya ufalme wako.

Kwa kumalizia, huu hapa uzuri wa ahadi ambazo maagano hutoa kwa wale wanaomchagua.

**Waefeso 5:30-32**

30 Kwa maana sisi tu viungo vya mwili wake, nyama yake na mifupa yake.
31 Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake,
ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja.
32 **Siri hii ni kubwa**, lakini **mimi nanena kuhusu Kristo na kanisa**.

Ushindi ulikuwa wake na wetu, mpango wote wa Mungu!

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com